

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM  
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI  
DAR ES SALAAM**

---

**MATANGAZO YA DOMINika YA 29**

**MWAKA C TAREHE 16 OCTOBA, 2022.**

**Kristo...**

**MCHANGO WA PILI**

Kwa ajili ya **UJENZI WA OFISI**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

**NDOA**

Bw. Florence Furaha mtoto wa Laurent Temba na Gloria Salim na Bi. Agness Kalisa mtoto wa Kalisa Blasio Kyaruzi na Shelestina Kamanzi.

**Tangazo la Pili.**

Bw.Paulo Samson Marwa Mtoto wa Samson Chacha na Christina Matinde na Bi.Pendo Joseph Siong'o Mtoto wa Joseph Siong'o na Rhobi Ngoko.

**Tangazo la Tatu na la mwisho.**

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

**UZINDUZI WA KWAYA YA MT. YOHANE PAULO WA II**

Kwaya ya Mt. Yohane Paul ii ya hapa Parokiani inatarajia kufanya uzinduzi mkubwa wa Albam yake mpya iitwayo "Mwalimu wangu" iliyo katika mfumo wa video na audio, siku ya jumapili ya tarehe 23/10/2022.Uzinduzi utafanyika katika misa ya kwanza na ya pili.Waumini wote tunakaribishwa kuwaunga mkono katika kuinua kazi hii nzuri ya kumtangaza Kristu kwa njia ya uimbaji.

**UWAKA**

uongozi wa Uwaka wanamshukuru Mungu kwa kuwawezesha kufanikisha ziara ya visiga kwa dada wadogo hapo Juzi..Wanamshukuru Baba Paroko na wana uwaka wote kwa pamoja kwa kujitoa na kuchangia vipaji.Jumla ya mahujaji 86 walishiriki na kutoa vipaji vyenye thamani ya shilingi 760,000 na mchango wa shilingi milioni tisa hivyo kushika nafasi ya Pili kijimbo na ya kwanza Kidekania.

**VIJANA**

Consolata Mission Centre Bunju wameandaa mafungo ya kmisionari kwa vijana wote, yatakayofanyika Consolata Mission Centre Bunju tarehe 22/10/2022.Safari itaanzia hapa Parokiani saa 1:00 asubuhi.Gharama kwa kila mshiriki ni shilingi 11,000 ambayo ni kwa ajili ya chai,chakula cha mchana na usafiri wa kwenda na kurudi.Kwa maelezo Zaidi waone uongozi wa vijana kwenye meza ya mauzo hapo duka la wawata.

**UCHAGUZI**

Kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa kwaya za Mt.Maria de Mattias na Kristu Mfalme Dominika ya tarehe 23/10/2022 na kwaya ya Mt. Yohane Paul II Dominika ya tarehe 30/10/2022 mara baada ya Misa ya kwanza.Wasimamizi wa uchaguzi

Deus Magala, Leonard Makungu ,Veronika Masawe, Shukuru Nyagawa, Benedictor Mlingi na Fulbert Mbando waonane na Uongozi wa Halmashauri ya Walei Parokia mara baada ya Misa.

### **ST GASPER VOCATION TRAINING**

Wamisionari wa Shirika la Damu Aziz ya Yesu wanatangaza nafasi za masomo katika chuo chao cha Mt. Gaspar kwa fani za Electrical Installation, Information Technology, Motor vehicle Mechanics,Carpentry,Tailoring and design, Catering,Driving na English course kwa maelezo Zaidi fika ofisi ya H/walei Parokia.

### **UFADHILI WA MAFUNZO YA PRE FORM ONE**

Kituo cha Kein Open School kilichopo Madale kinatoa ufadhili kwa wanafunzi wawili (wakike na kiume) kwa ajili ya kusoma kozi ya Pre form one.Kozi hii ni kwa wanafunzi waliohitimu darasa la saba 2022.Kwa maelezo Zaidi fika ofisi ya Parokia.

### **UJENZI**

Tunaendelea na kazi ya plasta eneo la nje ya jengo la ofisi kazi hiyo inategemewa kukamilia ndani ya mwezi huu.

### **USAIFI WA MAKABURI**

Kutakuwa na zoezi la usafi wa makaburi Jumamosi ijayo saa 12:30 asubuhi Hakutakuwa na sala za Jumuiya. Kanda ya Nazareti, Bethsaida na Kapernaum watafanya usafi makaburi ya Kwa Mponda. Kanda za Yerusalem, Bethlehem,Kana, Galilaya na Bethania watafanya usafi makaburi ya mtaa wa Hope.Tuje na vifaa vya usafi kama vile mapanga, fyekeo, reki na majembe. Pia tuje na rozari na sadaka.

### **WAWATA**

Kutakuwa na kikao cha Halmashauri WAWATA Parokia kitakacho fanyika leo mara baada ya Misa ya kwanza katika ukumbi wa Parokia.Walengwa ni viongozi wote watano wa kila jumuiya na watano wa Parokia.Hivyo viongozi wote mnaombwa kushiriki kikao hicho bila kukosa.

### **TANGAZO**

Masista wa Shirika la Mt. fransis wa Assisi wanapenda kuwatangazia wale wote wanaopenda kujunga na Shirika lao wawasiliane na masista hao. Kwa maelezo zaidi wawasiliane na Uongozi wa H/walei Parokia.

### **HUDUMA KANISANI**

Leo tunahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Teresia wa mtoto Yesu Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Mt.Yohane wa 23 Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Josephine Bakhita wajiandae

### **MAUZO**

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu.Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem.